Hakika umesema neno ambalo lau lingechanganywa na maji ya Bahari basi (lingeyabadili rangi) kwa kuchanganyika nayo

Imepokelewa kutoka kwa Aisha mama wa waumini radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Nilisema kumwambia Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Inakutosha kwa Safia kadhaa wa kadhaa, (Anasema mmoja wa wapokezi wa hadithi hii: Alikuwa akikusudia ufupi) Akasema: "Hakika umesema neno ambalo lau lingechanganywa na maji ya Bahari basi (lingeyabadili rangi) kwa kuchanganyika nayo" Akasema Aisha: Na nikamsimulia kuhusu mtu fulani, akasema: "Sipendi kuona kuwa kuna mtu nimemsimulia na kwamba mimi nina kadhaa wa kadhaa".

[Sahihi] [Imepokelewa na Abu Daud, Tirmidhiy na Ahmad]

Mama wa waumini Aisha radhi za Allah ziwe juu yake alisema kumwambia Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Inakutosha kwa Safia (Alikuwa akikusudia mama wa waumini radhi za Allah ziwe juu yake) Kuwa miongoni mwa aibu zake za kimaumbile ya kimwili ni mfupi, Mtume akasema: Hakika umesema neno ambalo lau lingechanganywa na maji ya Bahari basi lingeyazidia na kuyabadili na kuyaharibu, Aisha akasema: Na nilichokifanya ni sawa na kitendo cha mtu kumsema mtu ili kumshusha hadhi, akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Sipendezwi kuzungumza aibu zake, au kusimulia kuhusu yeye au kufanya mfano wa vitendo vyake, au kusema mfano wa kauli zake, kwa sura ya kumdharau hata kama nitapewa kiasi kingi katika mali za dunia kwa hilo.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3705